TANGAZO LA SERIKALI NA. 99 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA CHANG'OMBE YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Chang'ombe ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Nanyamba.

*Tangazo la serikali na. 99 (linaendelea)*

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH1 yenye majira – nukta 431497MS, 8791099KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $89^{0}$ 55'22'' kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH2 yenye majira - nukta 431891MS, 8791101KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $66^{0}$ 17'11'' kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH3 yenye majira - nukta 431997MS, 8791143KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $83^{0}$ 44'45''kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH4 yenye majira - nukta 432193MS, 8791163KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $85^{0}$ 27'07'' kwa umbali wa kilomita 0.14 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH5 yenye majira - nukta 432331MS, 8791156KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $17^{0}$ 41'04'' kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye makutano ya barabara ya Mtambaswala- Mangaka na mto Lidede kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH6 yenye majira - nukta 432384MS, 8790217KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $22^{0}$ 12'13'' kwa umbali wa kilomita 0.16 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH7 yenye majira – nukta 342484MS, 8790734KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya Mtambaswala- Mangaka hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH8 yenye majira - nukta 432385MS, 8790213KZ; baada hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata mto Lidede hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6th February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*